**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa unyenyekevu mkubwa natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambae ametujaalia kufika hapa kwa mara nyengine tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie wewe Mheshimiwa Spika busara, hekma na uadilifu katika kutuongoza na sisi pia atujaalie tuendelee kuwa na nguvu na ari ya kuitekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 pamoja na malengo tuliyojipangia ili tuweze kutoa huduma bora kwa Wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitakuwa mkosefu wa shukurani iwapo nitashindwa kuthamini juhudi za Mheshimiwa Rais za kuleta neema kwa wananchi wa Zanzibar kwa kutimiza ahadi zake ikiwemo ile ya kuongeza pencheni ambapo tumeshuhudia kwenye kilele cha Mei mosi Mheshimiwa ameongeza pencheni ya wastaafu kwa asilimia 100 na pencheni jamii kwa Wazee wetu kwa asilimia 150. Tunatoa pongezi za dhati kwa Kitendo hicho cha

kiungwana ambacho kimeibua hisia ya kuthaminiwa wazee wetu na faraja kwa jamii nzima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Makamo wa kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais kwa busara zao na ushauri wanaompatia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa mambo mbali mbali kwa ustawi wa nchi hii na wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee naomba nitumiye nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mheshimiwa Mudrik Ramadhan Soraga, Makatibu wakuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa juhudi wanazozichukua katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na mashirikiano yao ya dhati waliyoipatia Kamati wakati wote tulipokuwa tukipitia na kujadili mafungu ya bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na muundo wa Wizara hii kuwa na Makatibu Wakuu wawili (anaeshughulikia Uchumi na Uwekezaji) na (anaeshughulikia Kazi na Uwezeshaji), Kamati yangu ilipata fursa ya kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) na fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) siku ya Jumanne tarehe 02 Mei, 2023 na kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo pamoja na marekebisho madogo iliyoyapendekeza.

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kubwa ya kuipitia kwa kina Bajeti ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi Na Uwekezaji. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina wajumbe hao pamoja na Makatibu wao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti

2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan - M/Mwenyekiti

3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe

4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe

5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe

6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

7. Ndugu Nouman Thabit Nouman -Katibu

8. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima na taadhima, naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Uchumi kwa Programu Kuu na Programu ndogo za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imesikitishwa na mapungufu makubwa ya fedha kwa programu mbali mbali za Wizara hii. Kwa mfano, Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 10,766,374,000 kwa mwaka 2023/2024 ambazo ni mapungufu ya asilimia 63.3% kutokana na makadirio ya jumla ya shilingi za Kitanzania 29,377,207,000 za mwaka 2022/2023. Kadhalika, Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 2,459,437,000 kwa mwaka 2023/2024 ambazo ni mapungufu ya asilimia 37.95% kutokana na makadirio ya jumla ya shilingi za Kitanzania

3,963,913,000 za mwaka 2022/2023. Hivyo, tunaiomba Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuipatia Wizara hii kiasi kikubwa cha fedha zitakazoidhinishwa na Baraza hili, ili kukidhi utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kwa ufanisi.

**Fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu A07 linaloshughulikia Kazi na Uwezeshaji linakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 2,730,161,000 na kuchangia kwenye mfuko mkuu wa Serikali. Aidha, fungu hilo linakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 14,964,211,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za msingi. Hivyo, Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi inaishauri Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kukusanya na kutumia fedha hizo kwa uadilifu mkubwa huku ikijua kuwa matumaini ya vijana na wajasiriamali yapo kwa Wizara yao.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kutenga fedha zaidi kwa programu ndogo SA070201 ya Uratibu na Upatikanaji wa ajira za staha kwa wananchi wote. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu ndogo hiyo inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania milioni 200,000,000 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 25 ya fedha zilizopitishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambazo ni shilingi za kitanzania milioni 150,000,000.

Ongezeko hilo litasaidia kuratibu vyema masuala ya ajira kwa vijana wetu ili kufikia malengo yetu ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya kuwapatia vijana ajira 300,000 ifikapo mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imearifiwa kuwa kiwango cha ukosefu wa ajira kimeongezeka hasa kwa vijana kutoka asilimia 21.3 mwaka wa fedha 2014/2015 hadi asilimia 27.4 mwaka 2020/2021. Pamoja na mambo mengine, Kamati imebaini kuwa ongezeko hilo la ukosefu wa ajira nchini linachangiwa na kutokuwa na mpango maalum wa ajira wa Taifa. Kutokana na hali hiyo, tunaishauri Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar Kuandaa mpango mkakati wa ajira utakaokuwa ni dira kwa vijana wetu kujua ni fani gani ya kusoma ili kuajirika kwa urahisi sambamba na kuendeleza maslahi ya Taifa kwa kupata wataalamu wa fani zenye upungufu nchini na kuinusuru nchi yetu na matumizi makubwa ya fedha za kuwalipa wataalamu wa kigeni.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ndogo ya Usalama na Afya Kazini inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania milioni 420,000,000 kwa mwaka wa fedha 2023/2024, ikiwa ni upungufu wa milioni 30 kutoka kwenye makusanyo ya mwaka uliotangulia. Hali hii imechangiwa na upungufu wa vifaa vya ukaguzi kwa ajili ya kutoa huduma kwa Taasisi mbali mbali na upungufu wa wataalamu wa ukaguzi na hivyo kushindwa kufanya shughuli ya ukaguzi inavyostahiki. Aidha, Kamati imebaini kuwa Wizara hadi sasa imefanikiwa kufanya kaguzi za usalama kazini tu na kushindwa kulifanyia kazi suala la afya kazini ambapo hulazimika kutafuta wataalamu wa Wizara ya afya kupitia Hospitali ya Rufaa ya Mnazi mmoja kwa ajili ya shughuli hiyo na kukosa mapato yanayolipwa katika

eneo hilo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inaiomba Serikali kuipatia Idara ya Afya na Usalama kazini wataalamu na vifaa vitakavyoiwezesha kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya afya na usalama kazini ikiwa ni utimizaji wa majukumu yake ya msingi na kuongeza makusanyo ya Wizara.

## PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Mheshimiwa Spika,**

Kushuka kwa Programu kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (PA0703) ni suala linaloipa wakati mgumu Kamati yangu na kuibua maswali tofauti miongoni mwa Wajumbe. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hiyo inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za Kitanzania Bilioni 10,766,374,000 ambazo ni upungufu wa asilimia 63.3% kutokana na makadirio ya mwaka 2022/2023 ambazo zilitengwa jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 29,377,207,000.

Kamati yangu imesikitishwa sana na mapungufu hayo makubwa na kuiomba Serikali kuendeleza ajenda ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi ambayo inahitaji kulelewa kwa muda mrefu bila ya kuchoka ili tuyaone matunda yake kwa jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi Kwa mwaka wa fedha

2023/2024 unakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 9,014,952,000 kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za kuwalea na kuwahudumia wajasiriamali nchini. Fedha hizo ni chache mno kulingana na shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha. Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa kitendo cha Wakala kutumia njia mbadala za kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi na kuongeza juhudi za kuwahudumia wajasiriamali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kupitia programu ndogo ya Maendeleo ya Ushirika (A0712), Kamati inaipongeza Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kuongeza makadirio ya mapato kutoka Shilingi za kitanzania milioni 80,000,000 mwaka 2022/2023 hadi kufikia Shilingi za kitanzania milioni 150,000,000 kwa mwaka 2023/2024. Ingawa mapato hayo yameongezeka, Kamati yangu imearifiwa kuwa ada ya ukaguzi ni asilimia 5% ya faida inayotokana na chama husika ambapo pia imebaini kuwa mapato hayo hayakufikia kiwango stahiki kutokana na vyama vingi vya ushirika kutopata faida vyema. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Idara ya Usimamizi wa vyama vya ushirika kufanya ziara za mara kwa mara kwenye vyama ushirika na kuvipatia utaalamu kila inapohitajika kwa ajili ya kutengeneza faida zaidi.

**Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, fungu A08 linaloshughulikia Uchumi na Uwekezaji linakadiriwa kutumia jumla

ya shilingi za kitanzania bilioni 9,232,200,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake. Tunaipongeza Wizara kwa kutenga fungu hilo ili kuziwezesha shughuli za Uchumi na Uwekezaji kufanyika kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Ni jambo la kutia moyo sana kwa Kamati ya Uchumi kuarifiwa kuwa taratibu za ulipaji wa fidia kwa wahanga wa ujenzi wa barabara katika eneo la Uwekezaji Micheweni zinaendelea katika hatua za mwisho ambapo fedha za kulipia fidia hiyo tayari zimeingizwa kwenye akaunti ya Wizara. Kwa mnasaba huo, tunaiomba Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kulifanya jambo hilo haraka iwezekanavyo ili kuwapatia haki zao wananchi waliobakia na kuwaondolea msongo wa mawazo juu ya hatima yao.

**PROGRAMU KUU YA KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI**

**Mheshimiwa Spika,**

Mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ni nyenzo muhimu ya maendeleo ya nchi yetu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi za kitanzania milioni 484,076,000. Fedha hizo ni kidogo mno kulingana na jukumu linalobebwa na programu hiyo ndogo kwa uchumi wa nchi yetu.

Aidha, Kamati yangu imebaini kuwa miradi mingi ya PPP nchini hushindwa kufikia hatua ya utekelezaji na mara nyingi huishia njiani kutokana na kukosa upembuzi yakinifu (feasibility study). Kwa mnasaba huo, Kamati yangu inaiomba Serikali kuandaa (feasibility study) za miradi mbalimbali kabla ya kutafuta washirika wa kutekeleza miradi hiyo

ili kuwapata washirika hao kwa urahisi na kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Idara ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kuandaa miradi mitatu ya teknohama ambayo ipo kwenye hatua tofauti za maendeleo. Mradi wa Mkonga wa Taifa unaokadiriwa kujengwa kwa dola za Kimarekani milioni 44, Mradi wa Ujenzi wa Data center unaotarajiwa kutumia dola za Kimarekani milion 150 na mradi wa ujenzi wa digital platform kwa ajili ya wafanyabiashara kutangaza biashara zao mtandaoni. Kukamilika kwa Miradi hii kutasaidia kuwa na usalama wa taarifa za Serikali, kurahisisha mawasiliano baina ya taasisi za Serikali na kuwasaidia wafanyabiashara nchini kukuza biashara zao kwa njia za kisasa.

Mheshimiwa Spika,

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA) inakadiriwa kupokea ruzuku ya mishahara ya jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 2,887,800,000 Fedha hizo ni chache ikilinganishwa na mahitaji halisi ya ruzuku hiyo ya jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 3,328,000,000. Hivyo, Kamati yangu inaiomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuitatulia changamoto hiyo ili kuiwezesha ZIPA kufanya shughuli zake kwa ufanisi kwa maslahi ya Taifa.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS – KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**

**Mheshimiwa Spika,**

Kushuka kwa Makadirio ya matumizi ya Programu ndogo (SA080203) ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli zinazohusiana na Uchumi na

Uwekezaji Pemba ni jambo lililoishangaza Kamati yangu ambayo ilihoji juu ya uwezekano wa Ofisi ya Pemba kumudu gharama za uendeshaji kwa mwaka huu wa fedha. Jumla ya shilingi za Kitanzania milioni 144,799,000 zinakadiriwa kupungua kutoka kwenye programu ndogo hii ambayo mwaka 2022/2023 ilikadiriwa kupatiwa jumla ya shilingi za Kitanzania milioni 313,154,000. Kutokana na hali hiyo, Kamati ya Uchumi inaishauri Serikali Kuipatia Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji fedha zaidi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu ya Uchumi imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili watumie fursa hii kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili kumruhusu Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale waliyojipangia kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati yangu naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,



…………………………………………..

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**